

DMI: Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi azindua Bodi ya Magavana

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi, Dkt. Leonard Chamuriho amezindua Bodi ya Magavana ya Chuo cha Bahari Dar es salaam (DMI).

Uzinduzi wa bodi hiyo umefanyika jana tarehe 08.07.2021 baada ya bodi iliyokuwepo kumaliza kipindi chake cha miaka mitatu ambapo wajumbe wapya ni pamoja na Capt. Ernest Bupamba (Mwenyekiti), Dkt. Mwamini Tulli (Mjumbe), Capt. Andrew Tully (Mjumbe), Eng. Alfred W. Misana (Mjumbe) na Dkt. Erick P. Massami (Katibu)

Waziri Chamuriho, ameitaka bodi hiyo kutekeleza majukumu yake sambamba kabisa na mkakati wa serikali wa kuongeza mchango wa uchumi wa raslimali za maji (**Blue economy**) katika kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi wa Taifa

Alisema, anatarajia kuona kuwa chuo kinatekeleza majukumu yake katika namna ambayo itawezesha matokeo chanya ya mikakati iliyowekwa na serikali ikiwa ni pamoja na kutengeneza fursa za ajira katika sekta ya bahari na kupunguza umaskini wa kipato

Aidha, ameitaka Bodi ya chuo kutengeneza mpango kazi unaoakisi mkakati wa serikali kwa kuzingatia fursa zote zilizopo baharini katika kuongeza mchango wa uchumi wa raslimali za maji ili kuchochea uchumi wa nchi kupitia sekta ya bahari

Mhe. Chamuriho, amepongeza jitihada za chuo cha DMI kwa kusomeshasha wataanzania wengi ambao ni wataalam kwenye mambo ya bahari na kukitaka chuo kuwapatia majukumu ya kuihudumia sekta ya bahari ili Taifa liweze kufaidika ipasavyo na raslimali za maji.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi, Dkt. Leonard Chamuriho akizungumza na wajumbe wa Bodi mpya ya Magavana chuo cha DMI



Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Magavana ya Chuo cha Bahari – DMI, SPA. Dr. Mwamini Tully akitoa neno la shukrani kwa Mhe. Waziri wa Ujenzi.



Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es salaam, Dkr. Erick Massami akitoa neno la ukaribisho kwenye hafla fupi ya uzinduzi wa Bodi ya Magavana ya chuo cha DMI



Wajumbe wakiwa kwenye hafla fupi ya uzinduzi wa Bodi ya Magavana ya chuo cha Bahari Dar es salaam.



Waziri wa Ujenzi, Mhe. Dkt. Leonard Chamuriho (Kushoto) akikabidhi vitendea kazi kwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Magavana



Picha ya pamoja ya Mhe. Waziri wa Ujenzi na Wajumbe wa Bodi mpya ya Magavana ya Chuo cha DMI (Waliokaa) wakiwa na Wakuu wa Idara na Vitengo wa chuo cha DMI (Waliosimama).